# STD 7 END TERM 2 EXAM 2019

# KISWAHILI

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo kati ya yale ulivyopewa.***

Siku ya kurudi __1__ uliwadia. Wazazi wa Wambui __2__ naye kurudi shuleni. __3__ mwisho wa mwezi na magari ya abiria yalijaa __4__. Hata __5__, walifika shuleni salama __6__ Wambui alikuwa amejawa na soni. Hakutaka kumwona __7__ pale shuleni, __8__ wanafunzi. Hata hivyo alijikaza kwani __9__ lisilobidi __10__.

Walimu waliwaeleza wazazi wa Wambui __11__ mwana __12__ hatii bidii masomoni. __13__ anapotozwa na rafikiye aitwaye Shiro. Mamake Wambui akafoka, "Huyu mtoto wa kitajiri __14__ anayempotosha Wambui. Ni lazima aachane naye kabisa ili afaulu __15__ maisha yake.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. shule | B. skuli | C. skulini | D. shule ya |
| 2. | A. walianda | B. waliandamwa | C. waliandamana | D. waliondokaa |
| 3. | A. Ilikuwa | B. Palikuwa | C. Kulikuwa | D. Uikuwa |
| 4. | A. ndi | B. zi | C. pu | D. pomoni |
| 5. | A. hivo | B. hivyo | C. hilo | D. hizo |
| 6. | A. salama | B. salamu | C. aleikum | D. salimini |
| 7. | A. lolote | B. yeyote | C. chochote | D. wowote |
| 8. | A. hasa | B. kule | C. haza | D. hapo |
| 9. | A. alimaka | B. alidhani | C. alimaizi | D. alitafakari |
| 10. | A. hutenda | B. hutendwa | C. hutendeka | D. halitendeki |
| 11. | A. kuwa | B. kua | C. kwa | D. pakawa |
| 12. | A. yao | B. wao | C. zao | D. leo |
| 13. | A. Aidha | B. Eitha | C. Lakini | D. Kwingine |
| 14. | A. ndiye | B. ndilo | C. ndio | D. ndimo |
| 15. | A. kwa | B. kuwa | C. katika | D. kati |

***Kutoka swali la 16 hadi 30, chagua jibu lililo sahihi.***

16. ***Kanusha;-***

Angelitaka angelikusaidia.

A. Angalitaka angali kusaidia
B. Asingelitaka asingelikusaidia
C. Asingalitaka asingalikusaidia
D. Wangetaka wangekusaidia

17. ***Kamilisha methali;***

Mwenye macho haambiwi

A. enda
B. fanya
C. tazama
D. vizuri

18. Chagua neno baki.

A. mwamu
B. halati
C. wifi
D. shangazi

19. Mwana wa sungura huitwa

A. panya
B. kiluwiluwi
C. kimati
D. kitungule

20. Maana ya semi; Kula kalenda ni

A. kula chakula
B. kupigwa
C. kushikwa
D. kufungwa

21. Kitita cha kuni, kipeto cha

A. chawa
B. mchele
C. vitabu
D. barua

22. ***Chagua kivumishi;***

Mtoto mrefu ameenda nyumbani

A. mtoto
B. mrefu
C. ameenda
D. nyumbani

23. ***Kamilisha;-***

Makiwa ______________

A. poa
B. aheri
C. binuri
D. tunayo

24. Kiti kilivunjika ___________

A. trii
B. tang
C. kru
D. kacha

25. Ukubwa wa jiko.

A. kijiko
B. mko
C. jijiko
D. meko

26. Jina la akisami hii $^1/_6$ ni

A. subui
B. sudusi
C. tusui
D. thuluthi

27. Kati ya haya maneno ni lipi si kimelea?

A. kupe
B. nzige
C. kiroboto
D. mbu

28. Neno Mate liko katika ngeli ipi?

A. YA - YA
B. KI - VI
C. LI - YA
D. U - U

29. ***Tunasema;***

Mambo yalifanyika dhahiri ___________

A. shairi
B. shayari
C. shahiri
D. sairi

30. Ng'ombe ___________ wamepotea.

A. tisa
B. wakumi
C. wasaba
D. tatu

**Soma habari hii kisha ujibu maswali 31 - 40.**

Kuna jambo moja ambalo kila mtu mtaani kwao alikuwa analijua kumhusu Riziki. Riziki alikuwa na azma ya kuwa daktari. Waliijua nia yake kwa sababu Riziki alimwambia kila mtu aliyekubali kumpa masikio yake kumbikiliza. Watu wengi hasa marafiki zake shuleni, walimcheka tu.

Wengi waliyapuuza maneno yake kuwa ya mwofaji. Walimwona kama mtu anayeota vitu visivyowezekana kutokea. Angesomea wapi udaktari ilhali chuo kikuu kilichokuwa karibu kilikuwa takribani kilomita 600? Walishangaa. Huko ni mbali mno! Isitoshe, kulikuwa na madaktari wachache sana katika eneo lao. Hakuna hata daktari mmoja aliyetoka mtaa au mji wao. Wote walitoka katoka maeneo mengine. Jambo hili liliwafanya watu wengi mtaani kwao kudhania, kuwa kazi ya udaktari ni ya watu maalum, sio ya watu eneo lao. Hata hivyo, watu wazima pekee ndio waliomtia maanani riziki. Hawakulipuuza kamwe wazo la Riziki la kuwa daktari! Bali walimpa moyo.

Babake Riziki alikuwa mmoja wao, aliacha kitambo tabia ya kumfanyia mzaha mwanawe. Asubuhi ya siku moja alishinda nje ya nyumba yake akitengeneza kabati la mteja wake aliyeishi mjini. Hakuweza kujizuia kutabasamu alipofikiria ndoto ya bintiye ya kuwa daktari. Bwana Charo alijawa na huzuni na furaha wakati huo huo alipokumbuka namna ndoto hii ya Riziki ilivyozaliwa.

Ilianza miaka ishirini iliyopita. Riziki alikuwa na miaka wakati huo. Huu ulikuwa wakati mgumu kwa familia ya Charo. Katika kipindi hicho, mke wake alikuwa amepoteza kazi yake. Kuongezea dhiki juu ya dhiki, Tabu aliugua. Alikuwa mgonjwa sana hata wazazi wake Riziki wakawa hawajui la kufanya. Walishindwa jinsi ya kumsaidia kakake Riziki. Hali yao ya umaskini iliwafanya wahangaike huku na huko angalau wapate jirani mwema wa kuwasaidia. Babake Riziki alipita kila nyumba akitafuta usaidizi wa gari la jirani ambalo litampeleka hospitalini.

**31.** Riziki alikuwa na azma ya kuwa
- A. mwalimu
- B. mhasibu
- C. daktari
- D. mpishi

**32.** Ni kweli kusema kwamba Riziki aliweka azma yake
- A. kufuani
- B. kichwani
- C. bayana
- D. siri

**33.** Kicheko ambalo Riziki alipewa kilikuwa cha
- A. furaha
- B. huzuni
- C. dhihaka
- D. kupenda

**34.** Watu waliona matarajio ya Riziki kuwa
- A. kweli
- B. nyumba ya karatasi
- C. haraka
- D. mapewa

**35.** Changamoto kuu ya Riziki kuwa daktari ilikuwa
- A. uhaba wa vyuo vikuu
- B. kupasi mtihani
- C. uhaba wa wanafunzi
- D. pesa

**36.** Ukosefu wa madaktari katika eneo lao ulifanya watu wakadhani
- A. mtu hawezi kuwa daktari
- B. daktari si kazi ya wasichana
- C. udaktari ni kazi ya watu maalum
- D. daktari sharti atoke mbali

**37.** Ni watu gani waliompa Riziki moyo?
- A. jamii yake
- B. jamaa wke
- C. rafiki zake
- D. watu wazima

**38.** Baada ya madhila ambayo familia ilipitia yalimtia moyo. Ni methali ipi inadhihirisha haya?
- A. Aliye juu mngojee chini
- B. Baada ya dhiki ni faraja
- C. Zingwizingwi lipe nguo uone mashano
- D. Bandu bandu humaliza gogo

**39.** Kisawe cha umasikini ni
- A. utajiri
- B. uchochole
- C. uhayawani
- D. ukiwa

**40.** Kichwa mwafaka cha habari hii ni
- A. Baada ya dhiki faraja
- B. Penye nia pana njia
- C. Haraka haraka haina baraka
- D. Pole pole ndio mwendo

***Soma habari hii kisha ujibu maswali 41 - 50.***

Chungu hakumtilia maanani panzi. Aliendelea tu na kazi yake, "Mimi ninaweka akiba ya chakula kabla ya msimu wa masika au mvua kubwa kuanza. Nikiweka akiba ya chakula pamoja?" Chungu alimuuliza panzi.

"Msimu wa mvua bado uko mbali, na kuna chakula tele shambani. Kinatosha leo, kesho, kesho kutwa, mtondo, mtondogoo na hata baadaye. Bado kabisa wakati wa kufanya kazi,"Panzi akajibu.

Panzi aliendelea kucheza na kuimba. Siku nyingi zikapita. Panzi alikuwa na tabia ya uvivu. Chungu alikuwa na sifa ya bidii katika kazi. Kila siku alikusanya chakula kwa wingi na akakiweka nyumbani mwake.

Miezi ilipita kama maji. Katika mwezi ya Aprili hali ya anga ilianza kubadilika. Badala ya rangi ya samawati, mawingu meusi ya mvua yalianza kuenea kila upande na kuliziba jua. Kukawa na giza kama wakati wa magharibi. Umeme ulimeta mara kwa mara na kufwatwa kwa radi na mingurumo. Mvua yenye matone makubwa ikaanza kunyesha kwa kelele juu ya mapaa ya mabati. Wadudu walijificha kukimbia mvua na baridi. Panzi mvivu alitafuta chakula huku na huko bila mafanikio. Aliacha kuimba kwa kuzidiwa na njaa.

41. Kutokana na sentensi ya kwanza tunaweza sema kwamba chungu alikuwa
    A. mkaidi
    B. mvivu
    C. mwenye uroho
    D. mwenye bidii
42. Msimu ambao chungu alikuwa anajua hali itakuwa si hali ni upi?
    A. Masika
    B. Kipupwe
    C. Vuli
    D. Kiangazi
43. Chungu alitaka wapate kufanya nini?
    A. Kuhama sehemu hiyo
    B. Kujenga kichukuu
    C. Kupanda miwa
    D. Kushirikiana kuhifadhi chakula
44. Kwa nini panzi hakushirikiana na rafikiye?
    A. Alikuwa na hifadhi tosha
    B. hakukuwa na dalili ya masika
    C. masika ilikuwa mbali
    D. wakati wa masika ndipo kuna chakula
45. Panzi alijivunia chakula kipi?
    A. Kilichokuwa ghalani
    B. Kilichokuwa kwenye hifadhi
    C. Kilichokuwa sebuleni
    D. Kilichokuwa mashambani
46. Uraibu wa panzi ulikuwa ni nini?
    A. Kula
    B. Kulala
    C. Kuimba
    D. Kuimba na kucheza
47. "Miezi ilipita kama maji" ni mbinu ipi ya lugha?
    A. Istiara
    B. Methali
    C. Tashbihi
    D. Kitendawili
48. Mawingu yaligeuza rangi yakawa
    A. samawati
    B. kijivu
    C. hudhurungi
    D. meusi
49. Wakati wa magharibi ni upi?
    A. Mchana
    B. Usiku
    C. Jioni
    D. Hadhuhuri
50. Panzi alijuta kwa njaa na kujisikitikia kuwa laiti angelijua angelisikia
    A. la wazazi wake
    B. wakubwa wake
    C. wadogo wake
    D. la mwadhini na mteka maji msikitini